# RADIO INSTRUCTION TO STRENGTHEN EDUCATION (RISE)

NA

# ZANZIBAR TEACHER UPGRADING BY RADIO (ZTUR)

**Tathmini baada ya Mradi - Zanzibar**

Ripoti ya Mwisho

Januari, 2015







# UFUPISHO WA TAARIFA

## USULI WA MIRADI YA RISE NA ZTUR

Miradi ya Uimarishaji wa Elimu kwa njia ya Redio na Uinuaji wa Viwango vya Walimu kwa njia ya redio ilianzishwa Zanzibar Mwaka 2006. Miradi hii iliendeshwa kwa mfululizo hadi kufikia mwaka 2011 ikiwa na malengo yafuatayo:

1. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara Ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwenye fani ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto – ambayo inatafsiriwa kuwa ni kutoa huduma kwa watoto wenye umri wa mpaka kufikia miaka 8, na zinahusisha skuli za maandalizi na za darasa la 1 na 2 katika Mfumo wa Elimu ya Zanzibar.
2. Kuimarisha upatikanaji bora wa hesabati, kusoma, na stadi za maisha na vifaa kwa watoto wanaokosa huduma kwa urahisi (skuli za maandalizi hadi wale wa darasa la pili); na
3. Kutengeneza programu za mafunzo ya elimu masafa yaliyo bora na huria, yatakayowawezesha walimu wa maandalizi kukuza ujuzi wao, na kufanya kazi ili kuweza kutambulika katika masuala ya maandalizi.

Mradi wa "RISE" ulitekelezwa kwa ushirikiano baina ya Kituo cha Education Development Center, Inc (EDC) na Wizara Ya Elimu na Mafunzo ya Amali – Zanzibar kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Watu Wa Marekani (USAID). Shughuli za RISE zilitekelezwa katika wilaya mbili za Zanzibar ambazo zilikuwa zikipata matokeo ya chini kabisa ya masomo na baadaye shughuli hizo zilipanuliwa zaidi na kuingizwa kwenye programu ya mafunzo ya kuinua viwango vya walimu wa Zanzibar kupitia ZTUR.

Shughuli muhimu za utekelezaji chini ya mradi wa "RISE" ni:

- Kuandaa na kufanyia majaribio ngazi tatu ya vipindi vya mafunzo vya *TuchezeTujifunze*[1]*(TuTu)* kwa njia ya *Interactive Audio Instruction (IAI)*[2] kwa ajili ya wanafunzi wa maandalizi, darasa la 1 na 2, wakiwamo walioko katika mazingira rasmi na yasiyo rasmi ya kujifunza, ikiwa ni pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia;

[1] *TuchezeTujifunze*, ni jina linalotumiwa kwa vipindi shirikishi vya redio "IAI".
[2] IAIni mbinu shirikishi inayokuza ubora wa kujifunza katika mazingira tafauti,ikiwa ni pamoja na yale yenye upungufu wa walimu wasiokuwa na sifa,majengo na samani za skuli, na vifaa vya kujifunzia. Ikiwa ufundishaji wa kirafiki kwa watoto, ambayo ni jumuishi, ya ucheza, yenye vitendo, na inayoshirikisha, kila dakika 30 za kipindi zinatumia mtaala wa Kizanzibari kama msingi wa masomo (Kiswahili, Hesabu, Kiengereza na Stadi za Maisha), lakini inaoanisha michezo, nyimbo,na vitendo kutokana na hadithi hiyo hiyo moja. Vipindi vya IAI vinashajiisha utatuaji wa matatizo pamoja na wanafunzi kujiongoza kujifunza.

- Kuanzisha zaidi ya vituo 180 vya mafunzo ya awali ya mtoto vya Tucheze Tujifunze (Vituo vya TuTu) katika maeneo ambayo upatikanaji wa elimu, pamoja na elimu ya awali bado ni duni.
- Kuandaa video shirikishi kwa ajili ya kutoa miongozo ya kuwaimarisha walimu katika ufundishaji wa Kiengereza kama lugha ya pili.
- Kutoa mafunzo kwa kada ya walimu wa skuli za maandalizi na wa madarasa ya awali ( walio rasmi na wasio rasmi)ili kuwawezesha kufundisha kusoma, hesabati na stadi za maisha; na
- Kuijengea uwezo timu ya WEMA katika kusimamia usomaji kwa njia ya elimu masafa na huria kwa wote.

Hadi wakati mradi ulipokuwa unafungwa, RISE ilishatoa fursa za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Elimu ya Awali kwa watoto[3] wa Kizanzibari zaidi ya 35,000; na ilishatoa mafunzo kwa walimu zaidi ya 809 walio rasmi na wasio rasmi katika nyanja za ufundishaji za IAI, usimamizi wa darasa na nyanja nyengine muhimu. Aidha mradi uliweza kusambaza vifaa vya kujifunzia na kufundishia zaidi ya 28,000 vilivyoandaliwa na timu ya mradi.

Baadaye mradi wa ZTUR ulibuniwa kwa minajili ya kukuza kazi ya RISE katika Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya Mtoto kwa kuandaa programu (ya cheti) inayojitosheleza ya kuwajengea uwezo walimu wa elimu ya awali/maandalizi, itakayotekelezwa na WEMA. Lengo la programu hii (Programu ya Mpango wa Kuendeleza Elimu ya Watoto - *ECACP*) ni kuwapatia walimu waliko kazini maarifa muhimu, ujuzi na vitendo kupitia utaratibu wa elimu masafa unaosimamiwa katika Vituo vyao vya kupata huduma vya Walimu vya Wilaya. Programu ya *ECAP* inajumuisha vifaa vya sauti, video na vitabu ambavyo vinawaongoza walimu kupitia mafunzo ya nadharia na vitendo ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, na kuwasaidia wakati wanapokuwa wanafundisha madarasani.

# MALENGO YA UTAFITI

Mwaka 2014 EDC ilitoa kazi ya kufanywa utafiti wa baada ya mradi kumalizika ili kupata majibu ya maswali yafuatayo:

1. Ni kwa kiasi gani shughuli za mradi wa ZTUR na RISE ziliendelezwa au kupanuliwa chini ya usimamizi wa WEMA baada ya miradi hiyo kupelekwa huko Wizarani Machi 2011?
2. Je wanafunzi walioshiriki katika programu *ya IAI* (Tucheze Tujifunze) walifanya vizuri walipomaliza elimu yao ya msingi ukilinganisha na wale ambao hawakushiriki?

[3]Ifahamike kwamba zaidi ya wanafunzi 35,000 walifikiwa na mradi. Hata hivyo, kwa vile wanafunzi wengine walipata mafunzo kwa zaidi ya mwaka mmoja (maandalizi, Darasa la 1 na Darasala 2)hivyo jumla ya wanafunzi wote kwa mwaka ni 44,843.

Utafiti ulitumia mbinu changamano (tathmini ya mchakato mzima na athari zake) ili kupata majibu ya maswali haya. Mchakato wa tathmini ulizingatia ni kipi kiliendelezwa, kiliendelezwa vipi na ni changamoto na mafanikio gani ambazo WEMA ilikabiliana nazo wakati wa utekelezaji wake. Mahojiano na uchunguzi vilifanyika baina ya mwezi Machi na Juni 2014 kwa watu 94, wakiwemo maofisa wa WEMA kutoka ofisi za elimu za Wilaya na Makao Makuu ya Wizara, wafanyakazi wa Vituo vya Walimu, walimu wakuu wa skuli zilizojumuishwa katika programu za RISE, walimu ambao walipatiwa mafunzo kwenye programu ya Tujifunze Tucheze pamoja na wanafunzi waliosikiliza vipindi vya programu. Habari zilifanyiwa uchambuzi wa kimaelezo ili kupata maelezo yanayolingana ambayo yanajibu maswali ya utafiti.

Tathmini ya athari inaangalia ufaulu wa matokeo ya mwanafunzi wa darasa la 7 (ambao ni sawa na ngazi ya 7 kwa Marekani) katika masomo ya Kiswahili, Kiengereza na Hesabati. Zana ya utafiti iliandaliwa na timu ya tathmini kwa kutumia mitihani ya serikali ambayo imekuwa ikifanyika. Aidha sampuli iliyotumika katika kutafuta habari mwaka 2014, ni ya wanafunzi wale wale walioshiriki katika tathmini ya awali ya mwaka 2008 (wakati huo wakiwa wako darasa la kwanza). Katika jumla ya wanafunzi 1,543 kutokana na sampuli iliyotumika mwaka 2008, 904 (au 58.6%) walifanyiwa majaribio katika mwaka 2014; ikiwa ni pamoja na kikundi cha wanafunzi 552 wa *RISE,*(wale waliokuwa wakisikiliza vipindi vya *Tucheze Tujifunze*), na wanafunzi 352 walikuwa katika kikundi cha kulinganisha (wale waliokuwepo katika wilaya zenye mazingira yaliyofanana ambao hawakupata vipindi vya *TuchezeTujifunze* moja kwa moja). Si wanafunzi wote walifanyiwa majaribio mwaka 2014 walikuwa darasa la 7; habari za tathmini kwa wale waliokuwa madarasa ya chini hazikuingizwa katika uchambuzi wa matokeo ya tathmini kwa vile majaribio yalifanywa kutambua ujuzi kwa wanafunzi wa darasa la 7.

# YALIYOJITOKEZA

## UHAMISHO NA UENDELEVU WA MIRADI YA RISE NA ZTUR KITAASISI

Mafanikio makubwa ya miradi ya RISE na ZTUR yalijumuisha uanzishwaji kitengo cha elimu masafa na huria (Kitengo cha eLearning) ndani ya WEMA, kwa mafanikio. Kitengo cha eLearning kina wafanyakazi ambao walipatiwa mafunzo na kusaidiwa na RISE na ZTUR, ambapo utaratibu huu umekiwezesha kitengo kuendeleza baadhi ya shughuli zilizoasisiwa na miradi hiyo. Mpaka kufikia mwaka 2014, kitengo cha eLearning kilikuwa na wafanyakazi wataalamu 14, na shughuli zao (ambazo bado zinaendelea kufanywa kama shughuli zilizoasisiwa chini ya miradi ya RISE na ZTUR) zilikuwa zikipata msukumo zaidi kwa msaada wa Shirika la Misaada Ya Masuala ya Elimu Ulimwenguni (Global Partnership for Education). Hadi kufikia mwaka 2016, vituo vipya 120 (60 Mkoani Pemba na 60 Kaskazini B Unguja) vitakuwa vimeshafunguliwa, mafunzo na vifaa vitatolewa kwa wasaidizi 240 na vipindi 200 vya skuli mpya za maandalizi vitarikodiwa.

Mpaka kufikia mwaka 2014, vituo 179 kati ya vituo vya asili 180 vya *Tucheze Tujifunze* bado vilikuwepo, na juhudi mbali mbali zimechukuliwa katika kusaidia kujenga vyumba zaidi vya kudumu kwa vituo ambavyo havikuwa katika vyumba vya kudumu. Posho ya wasaidizi wa vituo vya TuTu zimeingizwa kwa ukamilifu kwenye bajeti ya Mwaka ya WEMA, ongezeko la posho ya wasaidizi hao mwaka 2013 ni ushahidi tosha wa juhudi na uwajibikaji wa kitengo katika ku endeleza kuwasaidia wasaidizi wake.

Urushaji wa vipindi vya masomo vya TUTU unaendelea, ingawa ulisimama kwa dharura kwa muda wa miezi 4 mwaka 2014, wakati ambapo Radio Tanzania Zanzibar ilipokuwa ikifanyiwa marekebisho na kupewa uhuru zaidi. Vipindi vyote (vya skuli za maandalizi na msingi) hivi sasa vinaendelea kurushwa hewani na ZBC.

Walimu wakuu, walimu na wasaidizi wote walielezea umuhimu wa kuendelea na programu za vipindi vyaTucheze na Tujifunze. Wasaidizi wanaendelea kuongoza madarasa mbali mbali, ingawa kuna uhaba wa upatikanaji wa programu na vifaa na mazingira tegemezi ya nyenzo.

Utaratibu wa RISE wa kutoa mafunzo ya mara kwa mara haukuendelezwa, sababu kubwa ya hali hiyo ni kutokana na kutopatikana kwa fedha za kuendeshea mafunzo. Pamoja na hayo, mwanzoni mwa mwaka 2014 mradi wa RISE uliendesha warsha mbili za mafunzo kwa wasaidizi wa vituo vipya 51 vilivyoanzishwa. Ufadhili wa warsha hizo 2 za mafunzo ulitolewa na GPE.

Mpango wa kuendeleza Elimu ya Watoto (ECACP) ilisarifiwa na kuendelezwa chini ya mradi wa ZTUR, ilitekelezwa kwenye Vituo 7 vya Walimu mwanzoni mwa mwaka 2014.[4] Hivi sasa ufadhili unatolewa na GPE kwa ajili ya utekelezaji wa ECACP Zanzibar nzima. Hadi ripoti hii ilipokuwa inaandaliwa kulikuwa na walimu 350 kutoka wilaya zote ambao walikuwa wanashapata hatua ya kwanza ya mafunzo na wakufunzi 30 ambao tayari walishapata vyeti vya ECAP. Zaidi ya walimu washiriki 3000 wanatarajiwa kufaidika na mradi wa ECACP, kuanzia mwaka 2014.

Changamoto kubwa zinazokabili utekelezaji bora ziko katika udhibiti na upatikanaji wa nyenzo sambamba na ubora wa vifaa na vipindi/programu. Matengenezo na ubadilishaji wa redio, pamoja na urushaji wa vipindi ni vikwazo vikubwa kwa wasikilizaji. Suala la ukosefu wa uchapishaji na usambazaji wa vifaa vipya na uhaba wa nyenzo mbali mbali zinazohitajika kwenye mafunzo ya mara kwa mara na ufatiliaji pia ni mambo ambayo kwa njia moja au nyengine yanaathiri ubora na kuaminika kwa utekelezaji.

## UTENDAJI WA WANAFUNZI

Tathmini iliyofanywa mwaka 2008 ilionesha kuwa vipindi vya mradi wa RISE IAI na utaratibu wake viliongeza maarifa katika kujifunza kwenye maeneo rasmi na yasiyo rasmi ya Zanzibar ukilinganisha na kikundi kulinganisha. Washiriki wa mradi wa RISE walionesha kuwa na matokeo mazuri kwa majaribio ya masomo yote matatu

[4]Vituo ni pamoja na: Kiembe Samaki, Bububu, Mkwajuni, Dunga, Kitogani, Mizingani-Mkoani.

waliyopewa (Kiswahili, Hesabati na Kiengereza). Ingawa ilionesha kuwa wanafunzi kwenye madarasa rasmi walipata maarifa vizuri zaidi, hawakuwaacha mbali kimaarifa wale wanafunzi ambao hawakuwa kwenye madarasa rasmi. Pamoja na kuwa wanawake na wanaume walifaidika na mradi wa RISE, hali inaonesha kuwa kwa ujumla wanawake walifaidika kwa kiasi kikubwa zaidi. Tathmini iliyofanywa mwaka 2008 ilionesha kuwa uonishaji wa vipindi vya redio vya IAI na elimu ya awali ya mtoto si kwamba tu kuliwasaidia watoto wanaojifunza bali pia kuliimarisha ubora wao wa kujifunza.

Utafiti wa mwaka 2014 ulijumuisha 59% ya wanafunzi kutoka katika sampuli ya mwanzo. Wanafunzi zaidi (63.4%) kutoka skuli rasmi walipatikana na kuteuliwa kama sampuli katika utafiti huu kuliko kutoka katika kikundi kishirikishi (55.9%). Wanafunzi wachache zaidi wa mradi wa RISE wasio rasmi na wale kikundi shirikishi walichaguliwa na kuhusishwa kama sampuli ukilinganisha na wale walioteuliwa kutoka katika skuli za serikali. Mwishowe timu ya utafiti iliamua kujumuisha wanafunzi kutoka eneo lisilo rasmi la RISE na kuwaunganisha na sampuli nyengine kuunda kikundi mchanganyiko kwa ajili ya kufanya uchanganuzi.

Tathmini ya mwaka 2014 iligundua kuwa wanafunzi kutoka katika skuli zilizo rasmi waliotathminiwa kwa mujibu wa viwango vya tathmini walifanya vizuri zaidi kwenye masomo yaliyorekebishwa ya Kiswahili, Kiengereza na Hisabati ukilinganisha na wenzao kutoka katika kikundi la ulinganisho na kutoka katika kikundi mchanganyiko cha mradi wa RISE. Miaka sita baada ya shughuli zake mbali mbali, wanafunzi kutoka skuli rasmi za RISE walionesha kufanya vizuri kwenye dhana kwa ngazi na kiwango chao. Pamoja na hayo, kiwango cha ufaulu wa jumla katika somo la Kiengereza na Hisabati kilionesha kuwa ni cha chini miongoni mwa vikundi vyote vilivyotafitiwa.

RISE inaonekana kuchangia vizuri katika kutoa faida endelevu kwa wanafunzi wa skuli zilizo rasmi zilizoshiriki katika mradi. Kwa bahati mbaya, haikuwezekana kuwapata wanafunzi na wa kutosha wasio rasmi au kutoka katika programu zilizounganishwa ambao wangewezesha kutoa hitimisho madhubuti juu ya athari za programu kwa watu hao wote. Wanafunzi kiasi kutoka katika kikundi mchanganyiko cha RISE ama haikuwezekana kuwapata na kuwajumuisha kwenye utafiti, au walirudia madarasa na kwa hivyo isingewezekana kuwajumuisha katika uchanganuzi. Kwa vile wanafunzi hao wana hali ngumu, kutokana na wazazi wao kuwa na kiwango kidogo cha elimu au kuwa masikini, walikuwa ni walengwa muhimu wa kupewa kipaumbele cha pekee katika programu ya RISE, na muonekano wa faida za muda mrefu za programu kwenye ufaulu wao wa masomo kungesaidia maamuzi ya sera na jinsi ya kuendeleza utengenezaji wa programu kwa watu wa aina hiyo kwa kupitia kitengo cha eLearning cha WEMA. Tathmini ya ziada au tafiti zinazolenga hususan katika kikundi hiki cha wanafunzi zingesaidia zaidi.

# HITIMISHO

Pamoja na changamoto za kifedha na uratibu, ambazo ni kawaida kutokea pale miradi inayofadhiliwa na wahisani inapopelekwa katika taasisi rasmi inayohusika na mradi, lengo la WEMA kutumia RISE na ZTUR kama msingi wa kuimarisha elimu ya awali Zanzibar kwa muda mrefu limefikiwa kwa kiasi kikubwa. Kitengo cha eLearning kina mkakati wa kuhakikisha kuwa kinaendelea na kazi zake chini ya msukumo na miongozo kutoka katika uongozi wa WEMA. Wafanyakazi wa kitengo cha eLearning wamefanya juhudi kubwa za makusudi kuzikuza na kuziendeleza shughuli za mradi wa RISE na ZTUR na hatimaye kuhakikisha kuwa malengo ya miradi hiyo katika kuimarisha maendeleo ya awali ya mtoto yanakuzwa. Dhamira ya uongozi wa WEMA ya kuona kuwa kitengo cha eLearning kinabakia kuwa imara, kama kilivyokuwa chini ya miradi RISE na ZTUR, imeipa matumaini ya timu ya kitengo hicho kuendelea na kazi yao, jambo ambalo limeshajiisha wahisani wapya ambao wanaweza kuchangia katika kuendelea kuimarisha sekta ya elimu ya awali Zanzibar.

Kwa kuongezea, shughuli za mradi wa RISE zimetoa athari chanya na endelevu kwa wanafunzi ambao walishiriki katika programu hizi, kwa kuwapatia mafanikio ya matokeo ya kielimu miaka 6 tokea kutathminiwa kwa mafanikio yao ya awali. Jambo hili halina mushkeli hususan kwa kikundi chla wanafunzi kutoka katika skuli rasmi ambazo zilikuwa chini ya mradi wa RISE. Pamoja na hayo, matokeo ya waliyotathminiwa ya RISE na washiriki waliolinganishwa wakati wa tathmini, yalikuwa ya chini kwa kiasi fulani, ikilinganishwa na matarajio ya kitaifa ya ufaulu wa wanafunzi wa kiwango cha darasa la 7. Kwa kweli, kama ilivyoainishwa katika Sera ya Elimu Zanzibar na Programu ya Maendeleo Ya Elimu Zanzibar, ipo haja ya kufanya juhudi kubwa ili kuongeza asilimia yawanafunzi wa Kizanzibari watakaofikia viwango vya ufaulu vinavyokubalika kwa ngazi ya msingi na sekondari. Utafiti zaidi wa tathmini ungepaswa kufanywa juu ya athari za programu za RISE kwa wanafunzi wasiofaidika sana (kikundi kililomo katika mradi wa RISE ambalo sio rasmi/haliko skuli). Utafiti huu ungesaidia kuhakikisha kuwa mradi unaleta faida kubwa kwa kikundi hicho kadiri kinavyoendelea kuhusishwa kwenye programu.

Kwa kuzigatia, mazingira ya Zanzibar, utumiaji wa programu za redio/sauti IAI unabakia kuwa mkakati muhimu na ufaao kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa elimu ya awali iliyo bora, hususan katika wilaya ambazo zianakabiliwa na changamoto nyingi. Juhudi kubwa zinapaswa kuchukuliwa katika kutoa msukumo na miundo mbinu muhimu ili kuhakikisha kuwa progamu za TuTu zinazoandaliwa ni zenye ubora (hususan: kufikiria kwa makini kuzioanisha programu mbali mbali kwenye ratiba za skuli ambazo zinakuwa zimejaa vipindi, kuendelea kutoa msukumo endelevu na kuwaendeleza kitaaluma walimu na wasaidizi, sambamba na kuwepo kwa ufuatliaji na tathmini madhubuti ya programu kadiri zinavyoendelea kutolewa). Sambamba na uwekezaji wa ziada katika michakato hii ya kuhakikisha kunakuwepo na ubora wa programu, pamoja na WEMA kuhakikisha kuamua kuendeleza kazi ya kitengo cha eLearning, uimara na mafanikio yaliyopatikana chini ya miradi ya RISE na ZTUR ni vitu ambavyo vinaweza kuendelea kuendelezwa na kudumishwa.